




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI MBEYA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MCC/E.40/5/VOL. II/82

11/07/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya amepata kibali cha ajira Mpya cha tarehe **06 Aprili, 2023** chenye **Kumb.Na.97/228/01/ "TEMP"/06** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,Hivyo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi ifuatayo:-

2. MWANDISHI MWENDESHA OFISI II, NAFASI MBILI (2)

2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Waombaji wawe na cheti cha kidato cha Nne (form IV) au VI aliyehitimu mafunzo ya stashahada (DIPLOMA) ya Uhazili au cheti cha NTA level 6 ya Uhazili. Aidha, wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingereza maneno 80 kwa dakika moja na kupata programu za komputa za ofisi kama vile: word, Excel, Powerpoint, Internet, Email na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali.

2.2 MAJUKUMU

- (i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na siri;
- (ii) Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa;
- (iii) Kutunza taarifa na Kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine;
- (iv) Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi;

- (v) Kupokea majalada na kusambaza kwa maafisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika;
- (vi) Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika;
- (vii) Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali ; na
- (viii) Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya ofisi.

2.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya serikali yaani TGS C.

2. MASHARTI YA JUMLA


- i) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
- ii) Waombaji wawasilishe picha mbili za hivi karibuni.
- iii) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- iv) Waombaji waambatanishe nakala ya vyeti vya masomo na taaluma na cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha "Result slip" "Statement of results" "Provisional results" au "Transcript". **HAVITAKUBALIKA.**
- v) Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitahani la Tanzania (NECTA).
- vi) Kwa waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).
- vii) Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakoitwa katika usaili.
- viii) Waombaji waandike namba ya kitambulisho cha Taifa katika barua za maombi au waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- ix) **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 24/07/2023 saa 9:30 Alasiri.**

MUHIMU: Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zote zinazohitajika. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji la Mbeya,
S.L.P 149,
MBEYA.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.mbeyacc.go.tz .

Tangazo hili limetolewa na:-



John J. Nchimbi,

**MKURUGENZI WA JIJI,
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA.**

**MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI
MBEYA**